

## Mapenzi ya Ahlul-Bayt A.S.

74. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.** , *Al-Jami'ul-Saghir*, J. 1 Uk. 14:

*“Wafunzeni watoto wenu vitu vitatu: Mapenzi ya Mtume wenu, Mapenzi ya Ahlul-Bayt, usomaji wa Qur'an.”*

75. **Amesema Al-Imam Ja'far as-Sadiq a.s.**, *Bihar al-Anwar* , J. 74, uk. 354:

*“Mtu yeyote ambaye hawezi kutufanyia wema wowote sisi Ahlul-Bayt basi wawafanyie mema wafuasi wetu walio wema; na yeyote yule asiyeweza kutuzuru, basi wanaweza kuwazuru wafuasi wetu walio wema ambavyo thawabu za kutuzuru sisi zitaandikiwa.”*

76. **Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s.**, *Al-Kafi*, J. 1, Uk. 187:

*“Kwa kile kilicho bora kabisa kwa mja kumkaribia Allah swt ni utiifu kwake Allah swt, utiifu kwa Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.. na utiifu kwa **ulil Amr.**”*

Aliendelea kusema:

*“Mapenzi yetu (ya Ahlul-Bayt) ni Imani na chuki dhidi yetu ni kufr.”*

77. **Amesema Al-Imam Ja'far as-Sadiq a.s.** *Bihar al-Anwar* , J.27, Uk.91:

*“Kwa hakika zipo daraja za ibada, lakini mapenzi yetu, Ahlul-Bayt, ni ibada iliyo bora kabisa.”*